KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 21, Issue 3
28th Jumaadal Awwal 1433
20th Apr, 2012

USHUJAA NA MAFANIKIO YA *MA-SWAHABIYYAAT* (MASWAHABA WA KIKE)

Na: SHEIKH MAHMUD AHMAD GHADANFAR

Ma-Swahabiyyaat (Maswahaba wa kike) ndio waliokuwa wanawake watukufu waliokuwa katika wakati mmoja pamoja na Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Wao ndio waliokuwa wakombozi wema wa Uislamu waliotakaswa, na wakapewa taadhima kubwa katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم) pamoja na kupewa bishara yakwamba wataishi milele Peponi siku ya kiyama. Mafanikio yao na athari zinapatikana kwenye kila mazingira ya muda wenye maana makubwa katika historia ya Ulimwengu, pindi walimwengu wote watakapogeuzwa milele na milele.
Walikuwa ni mahodari kwenye Dini yao kama walivyokuwa mahodari katika siyasa, wakawa ni mashujaa kwenye vita kama walivyokuwa na amani katika ushawishi wao wa ulinganizi katika Mafundisho ya Uislamu.
Wanawake hawa watukufu walipatikana kwa nafsi zao kwenye viwanja vya vita wakiwa miongoni mwa waliokuwa katika nafasi za mbele za waliokuwa wakipigana Jihaad. Walikuwa wakipatikana kwenye majukwaa ya siyasa, kwenye nyanja za I'lmu, kwenye mahakama za kisheriya za ki-Islamu, kwenye mafunzo ya kisheriya, kwenye biashara na mambo ya ki-Ufundi, kwenye ukulima, kwenye utabibu na udaktari. Kwa mukhtasari ni kwamba hapakuwepo na mazingira yoyote ambayo hayakufaidika kutokamana na utaalamu wao, hikma zao na hata ukarimu ulioandamana na tabia zao njema.

MAFANIKIO YAO KATIKA DINI:

Miongoni mwa huduma nyingi ambazo mtu huweza kujitolea katika Uislamu, ni kupigana katika viwanja vya vita. Ni michache mno, iwapo ilipatikana, mifano ya ghera sampuli hiyo, kujitolea, kuwa na uvumilivu na ujasiri kushuhudiwa kwenye historia. Pindi makafiri walipowashambulia Waislamu katika vita vya Uhud, walisalia wafuasi wachache waliojitolea na kupigana pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Katika hali hii ya maafa, swahaba wa kike aitwae Umm 'Ammaarah (رضي الله عنها) alimkinga Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa mwili wake na kuwafukuza maadui kwa upanga wake pamoja na uta na mikuki. Wakati bibi Qaniah alipomkurubia Mtume (صلى الله عليه وسلم), yeye ndiye aliyepatwa na mashambulizi aliyokusudiwa nayo Mtume (صلى الله عليه وسلم). Alipata jaraha kubwa kwenye bega lake, lakini hivyo hivyo aliendelea kuwashambulia maadui kwa upanga wake. Lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa ameekewa ngome madhubuti, hakuna aliyeweza kupenya na kuibonyeza ngao yake. Katika vita dhidi ya *Musailamah al-Kadh-dhaab* alipigana kwa ujasiri mkubwa mpaka akapata majeraha takriban kumi na mbili na akapoteza mkono wake.
Katika vita vya Ahzaab (vita vya khandaaq), Swahaba wa kike Swafiyyah (رضي الله عنها) alionyesha ushujaa wa maarifa ya kijeshi katika kuhimili mashambulizi ya Mayahudi, na akafaulu kumkata kichwa mmojawapo wa Mayahudi. Katika vita vya Hunain, Umm Salim alitoka na kuwashambulia maadui kwa upanga wake. Katika vita vya Yarmook, Asmaa' Bint Abu Bakr, Umm Abbaan, Umm Hakeem, Khawlah, Hind na Mama yao Waumini Juwayriyyah (رضي الله عنهن) walionyesha ushujaa wao wa ajabu. Asmaa' Bint Yazeed (رضي الله عنها) aliwauwa wanajeshi wa maadui tisa.
Katika mwaka wa 28 baada ya Hijrah, Umm Haraam alihusika katika mashambulizi dhidi ya Cyprus.
Mama yao Waumini, 'Aaisha, Umm Salim na Umm Salit (رضي الله عنهن) walikuwa ni miongoni mwa wataalamu katikia kuwatibu waliojeruhiwa. Kwa kawaida Maswahaba wa kike (Swahabiyyaat) walikuwa wakijiunga na Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika misafara ya kijeshi katika nchi kavu na vilevile katika Bahari. Mbali na kuchukuwa hatamu za kivita, palikuwa na huduma nyengine nyingi walizokuwa wakifanya, kama vile kuwapa wanajeshi huduma ya kwanza, kuwashughulikia waliojeruhiwa katika uwanja wa kivita na kuwapa maji na vyakula watle waliojeruhiwa na wenye kiu. Wanaposimama bega kwa bega na wanajeshi na huku wakiwapa mishale, wakiwahudumikia waliojeruhiwa na kwa ujumla wakiwasaidia katika kuwapa nguvu wanajeshi. Pia walikuwa wakiwabeba Mashahidi (waliokufa) na walioumia mpaka Al-Madinah. Umm 'Atiyyah (رضي الله عنها) aliwahi kushiriki kwenye vita Saba, na akapigana katika utawala wa Khalifa 'Umar (رضي الله عنه), wanawake pamoja na watoto walisaidia kuwazika waliokufa.
Waliusambaza ujumbe wa Dini mpya na kwa kupitia kwenye mifano yao waliwasilimisha makafiri wengi wakawa Waislamu. Alikuwa ni Faatimah Bint al-Khattab (رضي الله عنها) aliyemsilimisha nduguye 'Umar Bin al-Khattab, aliyekuja akawa mmojawapo wa Maswahaba mahodari mno wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na mwenye Imani ya hali ya juu. Ni Umm Salim (رضي الله عنها) aliyemshawishi Abu Twalha (رضي الله عنه) na ni Umm Hakim (رضي الله عنها) aliyemsisitiza mumewe, Ikrimah akubali kusilimu. Umm Shareek Dosiah alishughulika pamoja na wanawake wa kabila la Quraysh kwa tahadhari kubwa katika kuusambaza Uislamu.
Hali nyengine ya kazi ya ulinganizi ilikuwa ni kuuhifadhi Uislamu katika

YALIYOMO
MASWAHABIYYAT 1 - 4
MAZISHI 3 - 4

asili yake ya kutakasika, na kuulinda dhidi ya mabadiliko ya aina yoyote, uchafu na mambo ya uzushi yawezayo kusambaa ndani yake kutokana na mila au utamaduni wa makabila yaliyoenea katika jamii. Kazi hii ya kuuhifadhi utakaso wa Uislamu iliyokuwa na umuhimu mkubwa ilitekelezwa na ma-Swahabiyyat wengi; akiwemo mwanamke maarufu miongoni mwao, Bibi 'Aaisha (رضي الله عنها). Katika mwaka wa 35 baada ya Hijrah, pindi alipouwawa Khalifa 'Uthmaan (رضي الله عنه) pakatokea zogo na vurugu kuhusu ni nani atakaekuja baada yake katika mstari wa Ukhalifa, yeye ndiye aliyeleta umoja baina ya Maswahaba kwa kuwashawishi Waislamu wa Basrah (Iraq) na Makkah. Kuongoza Swala na kuadhini, au muadhini wenyewe, ni suala jengine lenye umuhimu mkubwa katika maisha ya ki-Dini.

Ingawa wanawake hawawezi kuwaongoza wanaume katika swala, wanaweza kufanya hivyo (kuongoza swala) katika mijumuiko ya wanawake peke yao. Vilevile wanawake wengi katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم) walitekeleza majukumu hayo. 'Aaisha, Umm Salim, Umm Waraqah na Sa'dah Bint Qamaamah (رضي الله عنهن) ndiwo waliokuwa miongoni mwa wanawake mashuhuri katika mas'ala hayo. Kwa hakika, Umm Waraqah aliigeuza nyumba yake ikawa ndipo mahali pa kuswaliwa na wanawake; hapo palikuwa pakiadhiniwa na mwanamke kwa ajili ya jamaa ya wanawake peke yao, na Umm Waraqah akatekeleza majukumu ya Imaam katika kuongoza swala.

MAFANIKIO YA KI-SIYASA

Vilevile *ma-Swahabiyyat* (Masahaba wanawake) walitekeleza uwajibikaji wao katika mambo ya Siyasa. Khalifa 'Umar Ibn al-Khattab (رضي الله عنه) alikuwa akimthamini sana Bibi Shifaa' bint 'Abdullaah (رضي الله عنها) kutokana na taaluma yake ya ki-Siyasa na mazingatio ya hali ya juu ambayo mara kwa mara alikuwa akimtaka shauri. Mara nyingi alikuwa akimkabidhi majukumu ya halmashauri ya ki-Taifa yanayohusiana na biashara na uchumi. Kabla ya kuhama (Hijrah) kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuelekea Al-Madinah, makafiri walitaka kuizingira nyumba yake, alikuwa ni Ruqayyah Bint Saifee (رضي الله عنها) aliyemtahadharisha. Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akatoweka kwa siri na kuelekea Al-Madinah, na kumuacha 'Ali (رضي الله عنه) akiwa amelala kwenye kitanda chake. Uislamu umewapa wanawake haki nyingi sana za ki-Siyasa. Mwanamke amepewa haki ya hata kumuhifadhi adui, akipenda kufanya hivyo. Mwana Historia, Abu Daawud amepokea yakwamba Umm Hani (رضي الله عنها), ambaye ni Dadake 'Ali (رضي الله عنه) alimpa hifadha adui kafiri na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: *"Iwapo utamuahidi hifadha na usalama mtu yoyote, basi sisi tutasimama na wewe."*

Hii ni Sheriya ya Uislamu yakwamba Imaam au kiongozi atalazimika kushikamana na ahadi iliyotolewa na mwanamke.

MOSOMO, 'ILMU NA SANAA

Kuna mafunzo mengi sana, ambayo ni ufahamu ulio na umuhimu katika kuijua Misingi ya dini na Itikadi zake. Usomaji tafauti katika *Qiraat,* na tafsiri, *Shari'ah, Fiqh, 'ilmu ya Hadeeth*, yote hayo ni fanni muhimu katika masomo ya Dini ya ki-Islamu. Wanawake wengi wa ki-Swahaba walikuwa ni mabingwa katika utaalamu huo. 'Aaisha aliihifadhi Qur'an, kama ambavyo Hafswah, Umm Salamah na Umm Waraqah (رضي الله عنهن) walivyoihifadhi. Hind Bint 'Aseed, Umm Hishaam Bin Haarithah, Zaydah Bint Hayyaan; Umm Sa'ad Bint Sa'ad (رضي الله عنهن) walihifadhi sehemu za Qur'an kwa moyo. Walikuwa na kawaida za kutoa mihadhara kuhusiana na Qur'an. Na katika ufahamu wa hadeeth, wote walikuwa na wajuzi , lakini 'Aaisha na Umm Salamah ndiwo waliokuwa na ubingwa maalum wa kuzifasiri na kuzifafanua. Ahaadeeth 2,210 zimefungamana na 'Aaisha na 378 zilifungamana na Umm Salamah. 'Aaisha alikuwa ni mjuzi katika kuzifasiri na kuzieleza Ahaadeeth hizo kutokana na uhusiano wake na Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Mengi yaliyomo katika kitabu cha tafseer cha Swaheeh Muslim kuna riwaya zake. Asmaa bint Abu Bakr (dadake 'Aaisha), Umm 'Atiyyah, Umm Haani na Faatimah bint Qays (رضي الله عنهن) pia wana 'ilmu nyingi katika fanni za ahaadeeth. Katika mas'ala ya Fiqh ya Ki-Islamu fataawa za 'Aisha zinaweza kujaza mijeledi ya vitabu vyengi. Na mengine kama hayo yanapatikana kutoka kwa fataawa zilizohifadhiwa za Umm Salamah. Thamani kubwa za fataawa za Swafiyyah, Hafswah, Umm Habibah, Juwairiyyah, Faatimah (binti yake Mtume (صلى الله عليه وسلم)), Umm Shareek, Umm 'Atiyyah, Asmaa bint Abu Bakr, Laila bint Qaa'if, Khawlah bint Tuyait, Umm Dardaa', 'Athikah bint Zaid, Swahlah bint Sohail, Faatimah bint Qais, Zaynab bint Jahsh, Umm Salmah, Umm Ayman, Umm Yusuf (رضي الله عنهن) wanaweza kujaza mijeledi mengi ya vitabu. Vilevile 'Aaisha alikuwa amebobea katika 'ilmu ya mirathi, hata ikawa Maswahaba wengi watukufu na waliokuwa maarufu walimtaka ushauri kuhusiana na nukta muhimu za kisheriya. Mbali na kuwa ni mabingwa wa Sheriya ya ki-Islamu na wajuzi katika nukta zilizokuwa na usahali za fiqh, wanawake wa ki-Swahaba walikuwa na ujuzi na maarifa makubwa katika tanzu nyengine za ki-ilimu. Asmaa bint Yazid bin Sakan (رضي الله عنها) alikuwa ni mfasaha mkubwa wa kuzungumza; Asmaa bint Umais (رضي الله عنها) alikuwa ni maarufu katika kufasiri ndoto. Maswahaba wengi wa kike walitambulika kwa ujuzi waliokuwa nao katika ta'aluma za madawa na upasuaji. Aslamiah Umm Mataa'a', Umm Kabshah, Hamnah bint Jahash, Mu'aadhah, Ammaimah, Umm Ziyad, Rabi'a bint Mu'awath, Umm 'Atiyyah, Umm Salim (رضي الله عنهن) ni baadhi ya miongoni mwa wanawake hao waliotambulika kwa ujuzi wao. Hema la Rufaida Aslamiah (رضي الله عنها) lilitengenezwa kwa madhumuni ya mahali maalum pa kufanyiwa upasuaji, likiwa na vyombo vyote vinavyohitajika vya huduma hiyo; na hema hilo lilikuwa kando ya Msikiti wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) mjini Madinah.

Katika ta'aluma za usanii nao hawakuachwa mbali kwa hali yoyote ilivyokuwa. Baadhi ya washairi waliotambulika walikuwa ni kina Sa'adi, Swafiyyah, 'Atikah, Bint Zayd, Hind bint Athaathah, Umm Aiman, Kabashah bint Raafi'a, Ummaamah Maridiah, Hind bint Haarith, Zaynab bint 'Awaam Azdi, Maimoonah na Ruqayyah (رضي الله عنهن). Kitabu cha mitungo ya Mashairi kilichoandikwa na *Khansaa* ndicho kitabu bora miongoni mwa mas'ala hayo kilichowahi kuchapishwa.

VIWANDA, BIASHARA NA UCHUMI

Vilevile wanawake wa ki-Swahaba walitekeleza shughuli za utenda-kazi au kazi za ki-ufundi kama tuzijuavyo siku hizi. Ukulima, biashara, mauzo na uchumi, uandishi, kazi za uhariri, viwanda vya mashambani kama vile ufumaji, uzalishaji katika viwanda na utengenezaji wa nguo - haya yote yametajwa katika *Musnad* (ukusanyaji wa hadeeth) ya Imaam Ahmad. Ukulima haukuwa maarufu sana, lakini kwa mara nyingi ulikuwa ukitekelezwa

katika sehemu za vitongojini zilizokuwa na rutba nyingi kwenye mazingira ya Al-Madina, hususan na wanawake wa ki-Answaar. Miongoni mwa Muhaajireen, au Muhaajir kama walivyokuwa wakijulikana, Asmaa' pia alikuwa ni mkulima. Zama za kabla ya kuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) zilikuwa zikijulikana kwa jina la *zama za ujinga* (wa kutojua kusoma wala kuandika), lakini baadhi ya wanawake hawa wenye kuthaminiwa walikuwa wame-elimika na kuwa na utaalamu wa ki-Ufundi katika sanaa na mitindo ya kuandika na uchoraji. Shifaa' bint 'Abdullaah (رضي الله عنها) alijifunza kusoma na kuandika hata katika zama hizi za giza mpaka akaheshimika vya kutosha kwa ufundi wake kwenye sanaa hiyo. Hafswah, Umm Kulthum bint 'Uqbah na Karimah bint Miqdad (رضي الله عنهن), wote hao walikuwa ni wasomi. 'Aaisha na Umm Salamah (رضي الله عنهما) hawakujua kuandika lakini walikuwa wanaweza kusoma. Wote hao wawili walibarikiwa na fahamu za kustaajabisha na mabongo ya kudadisi; na kutokamana na mkuruba waliokuwa nao na Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم), ahaadeeth nyingi zilizokuwa swaheeh zilitokamana na wao. Baadhi ya *Swahabiyyaat* pia walikuwa ni wafanyi biashara. Bibi Khadija (رضي الله عنها) alikuwa mfanyi-biashara wa kike aliyefaulu sana mpaka akawa anatuma misafara ya kibiashara kuelekea nchi tafauti. Khawlah, Maleekah, Thaqafiyyah na bint Fakhariyyah (رضي الله عنهن) walikuwa wakifanya biashara za mafuta ya manukato (*'Itar*) kutoka sehemu za Mashariki. Saudah (رضي الله عنها) alikuwa na kiwanda cha utengenezaji wa ngozi. Mabinti wa ki-Answaar walikuwa wakitunga beti za mashairi katika sherehe za siku-kuu na wakiimba. Kulingana na hadeeth iliyopokewa na Fri'aah bint Ma'auth (رضي الله عنها), waliyasoma mashairi yao mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), aliyependezwa mno ya ujuzi wao wa kimasomo. Umm Salmah (رضي الله عنها) alikuwa akiisoma Qur'an kwa hukmu za Tajweed, ta'luma ambayo ni ngumu sana na inayothaminiwa. Kwahiyo, hapakuwa na shughuli katika mazingira yoyote za ki-Jamii au za ki-Utamaduni - zilizokosa kupata athari na usaidizi uliotokamana na kuwepo kwa wanawake hawa watukufu. Twamuomba Allaah Awarehemu roho zao! Allaah Atakuwa radhi nao nao watakuwa na radhi nae.

MAZISHI

HUKMU YAKE: Kuwazika waliokufa, hata kama ni makafiri, ni *fardh-Kifaayah*. Hayo ndiyo mafunzo ya Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) na Maswahaba zake (رضي الله عنهم), kama ilivyoashiriwa kwenye ahaadeeth nyingi katika mlango huu, ikiwemo kuwazika kwake makafiri baada ya vita vya *Badr*.

KUWAHUSU MAKAFIRI:

[**MAZISHI YAO]:** Katika mafundisho ya Sunnah za Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ni kwamba anapokufa Kafiri, itawapasa Waislamu waharakishe kumzika katika hali sampuli mbili:

A. Ikiwa hakuna Makafiri wengine wa kumzika, au
B. Iwapo mtu anaehusiana nae sana na mwenye mas-uliya juu yake ni Muislamu.

Imepokewa kutoka kwa 'Umar, Ibn 'Umar, Abu Twalha na Anas (رضي الله عنهم) yakwamba: "Baada ya vita vya Badr, Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaamuru wafuasi wake wawazike watwevu ishirini na Nne miongoni mwa Maqureysh waliokufa, kwa kuwapandanisha mmoja juu ya mwengine, katika mtaro mchafu mno katika uwanja wa Badr - isipokuwa Umayyah Bin Khalaf, ambaye mwili wake uliovimba ukiwa ndani ya nguo zake za kivita mpaka ukajaa. Katika kujaribu kumburuta, akaanza kukatika-katika vipande, kwahiyo wakamuacha mahali alipokuwa wakamfunika kwa takataka na mawe. Kama ilivyokuwa kawaida yake baada ya kushinda vita, Mtume (صلى الله عليه وسلم) hukaa kwa siku tatu kwenye mazingira hayo ya uwanja wa vita. Katika siku ya tatu altayarishiwa mnyama wake kwa safari ya kuondoka, akaanza kutembea na huku akifuatwa na Maswahaba zake, mpaka akasimama kwenye ukingo wa mtaro. Akaanza kuwaita na haliyakuwa walikuwa wameshaoza miili yao, tena kwa majina yao na baba zao, akisema: 'Ewe Abu Jahl Bin Hisham! Ewe 'Utbah Bin Rabi'ah! Ewe Shaybah Bin Rabi'ah! Ewe Walid Bin 'Utbah! Nyinyi hamutamani yakwamba mungelimuamini Allaah na Mtume wake? Kwa hakika, sisi tumezipata ahadi kutoka kwa Mola wetu kuwa ni za kweli; Jee, nyinyi mumezipata ahadi za Mola wenu kuwa ni za kweli?' Hapo 'Umar (رضي الله عنه) na wenzake wakamaka, 'Ni vipi unawazungumzia baada yakwamba wamekufa kwa siku tatu? Wewe wazungumza na miili isiyokuwa na uhai? Watasikiya vipi na Allaah (سبحانه وتعالى) amesema, **"Kwa hakika wewe huwezi kuwasikilizisha waliokufa".** Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu, 'Naapa kwa Yule ambaye nafsi ya Muhammad iko kwenye Mikono yake, wewe hunisikii niyasemayo vizuri kuliko wanavyonisikiya wao! Sasa hivi wao wananisikiya. Wallaahi, sasa hivi wao wanajua kwa hakika yakwamba niliyowaambia ni ya kweli. Lakini hawawezi kunijibu kwa chochote.'" Katika kuichambua hadeeth hii, Qatadah (رحمه الله) amesema: "Allaah (سبحانه وتعالى) aliwapa uhai ili wapate kuyasikiya maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), kama kuwasuta na kuwadharau, na kuwafanya wasikiye majuto kwa waliyoyafanya. 'Ali (رضي الله عنه) amesimulia yakwamba babake alipokufa, Abu Twaalib, alikwenda kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia, "Mjombako, mzee mpotofu, ameshakufa; sasa ni nani atakaemzika?" Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu, "Nenda ukamzike, wala usifanye kitu chochote cha zaidi mpaka urudi hapa." 'Ali akamalizia kwa kusema, "Nilioga na nikarudi kwake. Akaniombea Du'aa' nzuri-nzuri tena za thamani kubwa kuliko Ngamia wekundu na weusi." Mpokezi kutoka kwa 'Ali (رضي الله عنه) (Abu 'Abd ur-Rahmaan as-Sulamee) akaongezea: "Baada ya kuosha maiti, 'Ali alikuwa akioga." Hapa nukta iliyoko kwenye hadeeth hii ni kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakumtazii 'Ali kwa kufiwa na babake aliyekufa haliyakuwa ni mshirikina, jambo ambalo linaloweza kufanywa kuwa ni dalili dhidi ya kuwatazii Waislamu kutokana na kifo cha jamaa zao makafiri - licha ya kuwatazii makafiri. Imezidi kueleweka na kubainika kutokana na hayo yakwamba imependekezwa kwa wanaume wenye kutekeleza maziko yenyewe waoge baada ya kuzika. Utambue pia yakwamba hapana ishara yoyote katika riwaya iliyo swaheeh ya hadeeth hii yakwamba 'Ali alimuosha babake. Kwahiyo, haiwezi kutumiwa kama ushahidi wa kumuosha kafiri.

[MAKABURI YALIYOTENGWA]: Kulingana na mafundisho ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na waumini kuanzia zama hizo mpaka hii leo zinaashiriya yakwamba haifai kumzika Muislamu pamoja na kafiri kwenye maziyara mamoja, wala kafiri pamoja na Muislamu: Inatakikaniwa yawekwe maziyara tafauti kwa Waislamu na mengine kwa makafiri. Bashir Bin al-Khasaasiyah amepokewa yakwamba siku moja alikuwa akitembea pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) na huku ameshikana nae mikono, mara akamwambia, "Ewe Ibn al-Khasaasiyah! Mbona umepambazukiwa na kumlalamikia Allaah (kuhusu kuwa mbali na jamii yako)? Sasa hivi wewe uko hapa, na hivi watembea pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم)! Huku akiwa bado amemshikilia mkono Mtume (صلى الله عليه وسلم), akamjibu, "Babangu na mamangu

wawe ni kikombozi kwako, Yaa Rasoolullaah! Mimi sikupambazukiwa na kumlalamikii Allaah kwa chochote! Yeye alinifanyia mimi kila jambo zuri."
Walipokuwa wakitembea, walipita kando ya makaburi ya washirikina, mara Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema, *"Hawa wameyakosa mambo mengi mazuri* (mara tatu). Kisha wakapita kando kando mwa makaburi ya Waislamu akasema, "*Hawa wamejipatia mambo mengi mazuri."* (mara tatu). Mara macho yake yakamuangazia mtu mmoja aliyekuwa akitembea na viatu viwili baina ya makaburi, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia, *"Ewe mtu uliyevaa viatu! Ole wako! Vua viatu vyako."* Baada ya kumtambua kuwa alikuwa ni Mtume (صلى الله عليه وسلم), yule mtu akavua viatu vyake mara moja akaviweka kando.
Hadeeth hii inaashiriya yakwamba palikuwa na kipambanuzi cha wazi baina ya makaburi ya makafiri na yale ya Waislamu. Ibn Hazm alishikilia kuwa ni ushahidi yakwamba haifai kumzika Muislamu pamoja na mushrik, na kwamba hairuhusiwi kutembea na viatu katika makaburi.

MAHALI PA KUZIKWA [MAKABURINI]: Kwa kawaida, maiti wote huzikwa makaburini. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akizika Waislamu waliokufa katika makaburi ya al-Baqee. Kuna riwaya chungu nzima kuhusiana na mas'ala hayo. Zaidi ya hayo ni kuwa hakuna riwaya yoyote inayoashiria yakwamba *Salaf* yoyote alizikwa mahali kwengine pasipokuwa makaburini isipokuwa kwa hali makhsusi ambazo tutakazozieleza hapo mbeleni.

MAHALI PA KIFO: Kuna riwaya nyingi (*mutawaatir*) zenye kuthibitisha yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alizikwa kwenye nyumba yake, mahali ambapo alipofia. Jambo hili ni makhsusi kwake, kama ilivyoashiriwa na 'Aaisha (رضي الله عنها), aliyepokewa akisema yakwamba alipokufa Mtume (صلى الله عليه وسلم), Maswahaba walikhitilafiana kuhusu mazishi yake, mpaka Abu Bakr (رضي الله عنه) aliposema yakwamba amewahi kusikiya jambo fulani kuhusiana na mas'ala hayo kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), na alipitikiwa kwa kusahau hayo, ambayo ni, *"Allaah hakuwahi kuchukuwa maisha ya Mtume wake isipokuwa huwa ndipo mahali atakapozikwa."* Kwahiyo, alizikwa katika mahali lilipokuwa godoro lake.

UWANJA WA VITA: Mashahidi (Waislamu waliouwawa katika uwanja wa vita), hawapelekwi makaburini, lakini huzikwa mahali ambapo walipouwawa. Jaabir Bin 'Abdullaah (رضي الله عنه) amesimulia yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipotoka nje ya al-Madina kwa ajili ya kupigana na Mushrikeen (katika vita vya Uhud), babake alimwambia, "Ewe Jaabir Bin 'Abdillaah! Kwanini wewe hubaki nyuma al-Madinah upate kuona yatakayotutokea sisi. Kwa hakika, Wallaahi, lau kama si kwa kuchelea kuwaacha baadhi ya mabinti zangu (wanaohitaji msaada), ningelitamani uuwawe wewe kabla yangu."
Jaabir akaendelea kusimulia. "Nilipokuwa nikisubiri al-Madinah, shangazi yangu akaniletea (maiti ya) babangu na mjombangu, akiwanig'iniza juu ya sehemu mbili za Ngamia. Akaingia al-Madinah kutaka kuwazika kwenye makaburi yetu. Lakini akatokeza mtu mmoja akamwambia, 'Kwa hakika, wewe umeamrishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) uwarudishe waliouwawa na uwazike mahali walipozaliwa.' Basi tukawachukuwa na kuwarudisha na tukawazika mahali walipouwawa.

NDANI YA NYUMBA? Isipokuwa katika hali ya kipekee ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), hairuhusiwi kuwazika waliokufa kwenye nyumba. Amesema al-Haafidh: "Pana uwezekano usio na shaka yakwamba watu wengine wamekatazwa kufanya jambo hilo, kwa sababu kuzikana ndani ya nyumba huzigeuza nyumba hizo kuwa ni mahali pa kuzikana, jambo lenye kukataza kuswali ndani yake."
Al-Bukhaari ameyapata makatazo hayo kutoka kwenye hadeeth ya Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Swalini baadhi ya swala zenu ndani ya nyumba zenu, na musizigeuze kuwa ni makaburi."* Kulingana na al-Haafidh, hadeeth ya Abu Hurairah iko wazi zaidi kuhusiana na mas'ala haya, ikiashiria waziwazi yakwamba imeharamishwa kuzikana kwenye majumba: *"Musizigeuze nyumba zenu kuwa ni makaburi."*

NYAKATI ZA MAZISHI: [KUHARAKISHA MAZISHI]
Inapaswa kuharakisha katika matayarisho ya mazishi. Kwa kawaida Muislamu anatakiwa kuzikwa ndani ya muda wa masaa ishirini na nne kuanzia kufa kwake.
Kuchelewa kuzikwa makhsusi kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakufai kuchukuliwa kuwa ni mfano katika mas'ala haya. Alikufa siku ya Jumatatu (wakati wa mchana), akaoshwa na kuvishwa sanda siku ya Jumanne, na akazikwa wakati wa masaa ya katikati za usiku, na muda wote ukawa ni masaa thalathini na sita baada ya kufa kwake. Sababu ya kuchelewa huko ilikuwa ni mshtuko mkubwa wa Maswahaba kutokamana na tukio hilo la kuumiza, na pia kusitasita kwao mwanzoni kuhusu jinsi ya kumuosha, kumvisha sanda, na kumzika.

NYAKATI TATU ZILIZOHARAMISHWA: Haifai kuzikana katika nyakati tatu zilizotajwa kwenye hadeeth ya 'Uqbah Bin 'Aamir (رضي الله عنه): "Kuna nyakati tatu ambazo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alizotukataza kuswali au kuzika maiti zetu:
1. Jua linapochomoza - mpaka lipande juu.
2. Wakati wa mchana unapoanza mpaka Jua linapoanguka (kupita saa sita mchana), na
3. Jua linapokurubia kutwa - mpaka lizame.

MAZISHI YA USIKU: Vilevile, imeharamishwa kuzika usiku isipokuwa iwapo kutakuwa na dharura ya kufanya hivyo. Hii imetokamana na hadeeth ya Jaabir Bin 'Abdillaah (رضي الله عنه), aliposema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikataza mtu asizikwe katika wakati wa usiku kabla ya kuswaliwa - isipokuwa mtu atalazimika kufanya hivyo."
Sababu ya haya ni kwamba matokeo ya mazishi ya usiku ni idadi ndogo ya watu watakaoswalia maiti, kufuata jeneza lake na kumzika. Ni muhimu kupata idadi kubwa ya watu, kwa sababu ya faida na malipo mema watakayopata kwa kutekeleza uwajibikaji wa ki-Islamu kama huo, na pia kulifanya jambo hilo litakabaliwe katika maombi yao kwa maiti.
Amesema an-Nawawee: Ma'ulamaa' wamekhitilafiana kuhusu kuzikana katika nyakati za usiku. Al-Hasan al-Basree amesema ni makrooh, isipokuwa iwapo patakuwa na dharura. Hadeeth hii ndiyo dalili yake. Hatahivyo, wanavyuoni wengi wa zamani na wa sasa wamesema yakwamba si makrooh, kwa sababu Abu Bakr as-Siddiq (رضي الله عنه) na kundi kiubwa la ma-Salaf walizikwa katika nyakati za usiku bila ya pingamizi yoyote, na yule mwanamke mweusi na pia yule mtu aliyekuwa akisafisha msikiti, wote hao wawili walizikwa katika nyakati za usiku bila ya upinzani (wa hayo) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Ibn Hazm amejibu hoja hii kwa kusema, "Kwa kila aliyezikwa katika wakati wa usiku, awapo ni yeye mwenyewe (صلى الله عليه وسلم), wakeze, kuhofia jua kali katika wakati wa mchana ...

[ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO]